



## **Tulikuwa tukitoa kipindi alipokuwa nasi Mtume rehema na amani ziwe juu yake zakatul fitiri, kwa kila mdogo na mkubwa, huru au mamluki, kibaba cha chakula, au kibaba cha siyagi, au kibaba cha ngano, au kibaba cha zabibu**

Kutoka kwa Abuu Saidi Al-Kudry -radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Tulikuwa tukitoa kipindi alipokuwa nasi Mtume rehema na amani ziwe juu yake zakatul fitiri, kwa kila mdogo na mkubwa, huru au mamluki, kibaba cha chakula, au kibaba cha siyagi, au kibaba cha ngano, au kibaba cha zabibu, hatukuacha kuendelea kuitoa, mpaka alipokuja kwetu Muawia bin Abii Sufian radhi za Allah ziwe juu yake kwa ajili ya Hija, au Umra, akazungumza na watu katika Mimbari, ikawa katika yale aliyozungumza na watu alisema kuwa: Hakika mimi ninaona kuwa vibaba viwili vya kipimo cha kutoka Samraa ya Sham, vinalingana na kibaba kimoja cha tende, watu wakalichukua hilo, anasema Abuu Saidi: Ama mimi niliendelea kuitoa kama nilivyokuwa nikiitoa, milele kwa muda wote nilioishi.

[صحيح] [متفق عليه]

Waislamu walikuwa wakitoa zakatul-fitiri katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake na zama za makhalifa waongofu baada yake kwa mdogo na mkubwa, kiwango cha kibaba cha chakula. Na chakula chao kilikuwa ni ngano na (Zabibu): Zabibu kavu, na (samli): Maziwa yaliyokaushwa na tende. Na kiwango cha kibaba kimoja ni 'mudi' nne, na mudi moja inalingana na ujazo wa viganja viwili vya mtu aliyelingana sawa. Alipokuja Muawia radhi za Allah ziwe juu yake katika mji wa Madina akiwa Khalifa, na ngano ya Sham ilikuwa nyingi wakati huo, alitoa hotuba akasema: Hakika mimi ninaona vibaba viwili vya ngano ya Sham (ni nusu ya kibaba), vinalingana na nusu ya kibaba cha tende, watu wakalichukua hilo. Akasema Abuu Saidi Al-Khudri radhi za Allah ziwe juu yake: Ama mimi ninaendelea kutoa kama nilivyokuwa nikitoa katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake daima maishani mwangu.

النجاة الخيرية  
ALNAJAT CHARITY

